



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 06 Juni, 2017.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara
Maalum za SMZ:**

90. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kamishna Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar anastahiki pongezi kwa kazi kubwa aliyofanya ya kutengeneza vitanda kwa ajili ya wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo na hivi karibuni ameendelea na kazi hiyo kwa kutumia wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar.

Je, ni vitanda vingapi vinahitajika kwa ajili ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

129. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo ina wajibu wa kufanya utafiti ili kubaini aina mbali mbali za vifaranga vya samaki ambao wanaweza kufugwa. Na kwa kuwa maeneo mengi ambayo kwa Pemba yanaweza kufugia samaki kwa sasa ni sehemu za Majangwani ambayo kuna muingiliano wa maji ya chumvi na maji baridi hasa wakati wa mvua.

- (a) Je, ni aina gani ya vifaranga vya samaki ambavyo vinaweza kuishi vinapopatwa na maji baridi na samaki hao wasiathirike kabla ya kuingiliwa na maji ya chumvi ambayo ndio hasa yanayokusudiwa kwa ufugaji huo.
- (b) Je, vifaranga vya samaki Jodari, Nguru na Songoro ambao ni samaki wenye bei kubwa, wameanza kuzalishwa na pia wanaweza kuishi kwenye mazingira kama hayo tunayoyaulizia.
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wafugaji wa samaki wa kuwapatia mafunzo ya ufugaji samaki na mitaji.

Wizara ya Fedha na Mipango

95. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kwa wafanyabishara kulipishwa VAT mara mbili wakiwa Dar es Salaam na mzigo unapofika Zanzibar nako wanalipishwa VAT. Suala hili limekuwapo muda mrefu licha ya kudaiwa kushughulikiwa mara kwa mara lakini hakuna mabadiliko yoyote.

- (a) Serikali haioni kuwa mtindo huu ni sawa na kuwaonea au kuwakandamiza wafanyabishara.

- (b) Serikali haioni kuwa wakati umefika sasa kuafikiana na Ujamaa wa pili wa Jamhuri ya Muungano ili jambo hili linalokera sana likamalizwa.
- (c) Ni lini hasa jambo hili litafikia mwisho.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

157. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi sana kupunguza migogoro ya ardhi mpaka kufikia kuanzisha Mahakama ya Ardhi. Hata hivyo, bado suala hilo linaonesha ndio kwanza linakuwa kuliko kupunguwa ambapo inaonekana labda baadhi ya Sheria zimepitwa na wakati.

- (a) Je Serikali inalijua hilo.
- (b) Je, Serikali iko tayari kuzifanyia marekebisho baadhi ya Sheria za Ardhi ili kupunguza migogoro hiyo.
- (c) Je, Serikali imejipanga vipi kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya Ardhi inayoshamiri siku hadi siku.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

168. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kampuni ya Zantel imekuwa ni kielelezo cha huduma za mawasiliano kwa upande wa Zanzibar kwa miaka mingi sasa. Hata hivyo, kadri siku zinavyokwenda, huduma za Kampuni hiyo zimekuwa zikizorota mara kwa mara. Mara kadhaa mtandao huo hukatisha

mawasiliano bila taarifa, wakati mwingine mteja hukatwa fedha kwa huduma ambayo haifahamu, au makato yanatangulia kabla ya huduma haijaanza.

Je, nini tatizo linasababisha huduma za Kampuni hiyo kuzorota mara kwa mara na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko:

166. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Kwa muda mrefu sasa kiwanda cha soda cha Maruhubi kimefungwa na hakuna uzalishaji unaofanyika hapo hali inayopelekea soda kuagizwa kutoka Tanzania bara na pia Serikali kukosa mapato.

- (a) Je, Serikali ipo tayari kukiuzua au kukikodisha kiwanda kile kwa mtu mwingine kama ilivyofanya kwa viwanda vyengine.
- (b) Je, ni muda gani tangu kufungwa kwa kiwanda hicho.
- (c) Je, hasara gani imepatikana baada kufungwa kiwanda hicho.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa Mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
06 Juni, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.